TANGAZO LA SERIKALI Na. 280 La Tarehe 19/3/2021

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

***(****Imetungwa chini ya Vifungu vya 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA SOKO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA, 2021

Jina na mwanzo wa Sheria Kutumika

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Soko ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ya mwaka 2021.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa itakavyoelezwa vinginevyo:

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtu ambaye ameteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Chunya;

"kizimba" Maana yake ni jengo lolote, chumba, kioski au duka ndani ya soko au kuzunguka eneo la soko ambalo linatumika kwa madhumuni ya kuuzia bidhaa;

"Mkurugenzi"Maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya au mtu yeyote aliyeteuliwa kufanya kazi za Mkurugenzi;

"soko" Maana yake ni eneo lolote lililotengwa kwa ajili ya kuuza na kununua bidhaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na maduka, na vioski;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni Mtu, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Ushuru wa Soko

3.- (1) Halmashauri itaanzisha na kutoza ushuru wa soko kwa mtu yeyote atakayefanya biashara kwenye maeneo ya soko kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza mazao au bidhaa nje ya eneo la soko.

Mgawanyo wa Mapato

4. Asilimia 80% ya mapato yatakayokusanywa kwenye masoko na magulio yataingia kwenye mfuko wa Halmashauri na asilimia 20% kwenye mfuko wa serikali ya Kijiji ambapo soko au gulio lipo.

Wajibu wa kulipa Ushuru

5. Kila muuzaji wa bidhaa katika soko atalipa ushuru uliopangwa katika Sheria Ndogo hii kwa Halmashauri au wakala aliyeteuliwa na Halmashauri na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Muda wa kazi

6 Kila soko litakuwa wazi kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni.

Wakala

7.- (1) Halmashauri inaweza kutangaza zabuni ya ukusanyaji wa ushuru wa soko na kumteua wakala ikiwa ni mtu binafsi au kampuni, ambaye ataingia mkataba wa uwakala na Halmashauri ili kukusanya ushuru wa soko.

(2) Wakala atakayeteuliwa na Halmashauri kutekeleza jukumu lolote chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kusimamia jukumu hilo kwa viwango vilivyoainishwa chini ya Sheria Ndogo hii.

(3) Wakala aliyeteuliwa atakuwa na majukumu ya kukusanya ushuru na kumshtaki Mahakamani mtu yeyote atakayeshindwa kwa makusudi kulipa ushuru anaotakiwa kulipa.

Makosa na Adhabu

8.- (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

a) atashindwa kulipa ushuru;
b) atashawishi mtu au kundi la watu wasilipe ushuru;
c) atauza bidhaa nje ya maeneo yaliyotengwa kama soko;
d) atashindwa kuzingatia kanuni za usafi;
e) atachelewesha kuwasilisha ushuru kwa Halmashauri;
f) atakusanya ushuru zaidi ya kiwango kilichoanishwa kwenye Sheria Ndogo hii;
g) atauza au kununua bidhaa nje ya soko katika muda uliopangwa;
h) atauza mazao au bidhaa ambazo hazina viwango vya ubora zinaweza kusababisha madhara kwa afya.

(2) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kifungu kidogo cha kwanza atahukumiwa adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo

kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne.

Mamlaka ya Halmashauri kutoa mwongozo.

10 Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kutoa Mwongozo kuhusiana na Sheria Ndogo hii endapo kutakuwa na haja ya kufanya hivyo.

Kufililisha kosa

11. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ushuru anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

Limetengenezwa chini ya kifungu cha 3(1)

USHURU WA VIZIMBA SOKONI

| NA | AINA YA KIZIMBA | KIASI CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1 | Kizimba cha Matunda,Mboga na vitu vingine vya sokoni | Tsh. 500 kwa siku |
| 2 | Kizimba cha Nafaka, na vitu vingine vya sokoni. | Tsh. 500 kwa siku |
| 3 | Kizimba cha Bucha | Tsh. 500 kwa siku |
| 4 | Kizimba cha Chakula | Tsh. 500 kwa siku |
| 5 | Kizimba cha Mitumba | Tsh. 500 kwa siku |
| 6. | Maduka,vilabu na bar kuzunguka soko | Tsh. 500 kwa siku |
| 7 | Ushuru wa soko mnadani | Tsh, 500 kila muuzaji |

JEDWALI LA PILI

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 11*)

KUFILILISHA KOSA

Mimi……………………………………..………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, kwamba mnamo tarehe ………mwezi………. Mwaka………. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha………………. cha Sheria Ndogo ya Ushuru wa Soko ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ya mwaka 2021.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halamashauri ya Wilaya ya Chunya, Niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru ninayodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……………………………… ya Mwezi…………………. Mwaka…………………

Jina…………………………………………Saini………………………………………

Mbele ya:

Jina………………………………………...Cheo…………………………………….

Saini……………………………………Tarehe……………………………………

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya imebandikwa kwenye Sheria ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 30/6/2020:-

SOPHIA JUMA KUMBULI,
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Chunya*

MHE. BOSCO SAID MWANGINDE,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Chunya*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
22 Februari, 2021

SELEMANI SAID JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi -OR- Tamisemi*